

Unapofanya Mawasiliano

Simu ya moja kwa moja inaweza kukusaidia:

- Kuelewa tofauti baina ya uhalifu wa chuki na tukio la upendeleo
- Kufahamu chaguo na rasilimali zilizopo
- Kukuunganisha na huduma zinazozingatia waathirika, zinazoheshimu tamaduni na zenye kuelewa athari za kiwewe katika eneo lako

Unaweza kuwasiliana na Simu ya moja kwa moja kama ulipitia tukio hilo wewe mwenyewe au ulilishuhudia.

Kuhusu Hate Crimes & Bias Incidents Hotline

Simu ya moja kwa moja ni kituo cha taarifa zisizo za dharura na rufaa kinachosaidia watu walioathiriwa na uhalifu wa chuki na matukio ya upendeleo waweze kupata usaidizi. Huduma ya simu ya moja kwa moja inapatikana katika lugha nyingi, na ni ya siri. Huduma ya simu ya moja kwa moja huwasiliana tu na vyombo vya dola unapotaka iwe hivyo na kwa idhini yako.

Jinsi ya Kutoa Taarifa




855-225-1010

atg.wa.gov/report-hate



Utaunganishwa na mtu anayezungumza lugha yako.



Washington State Hate Crimes
& Bias Incidents Hotline

Ripoti Chuki. Pata Usaidizi.

Chuki na upendeleo vina athari kubwa kwa watu, familia na jamii. Washington State Hate Crimes & Bias Incidents Hotline (Simu ya Moja kwa Moja ya Uhalifu wa Chuki na Matukio ya Upendeleo Jimboni Washington) ipo hapa kutoa usaidizi kwa mtu yeyote aliyekabiliana au kushuhudia kitendo cha chuki.

Simu hii ya moja kwa moja hutoa usaidizi **bila malipo, kwa siri** jimboni kote. Huna haja ya kufahamu kama kilichotokea ni uhalifu. Tutakusaidia kuelewa chaguzi ulizo nazo.

Wasiliana na Simu ya Moja kwa Moja



855-225-1010

atg.wa.gov/report-hate



Inapatikana katika lugha nyingi

Huduma ya simu ya moja kwa moja ni ya siri, haina malipo, na inapatikana jimboni kote bila kujali hali yako ya uhamiaji. Sisi siyo polisi na hatutoi taarifa kwa polisi bila idhini yako.

Imetolewa na Washington State Office of the Attorney General (Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Jimbo la Washington).

Huduma ya simu ya moja kwa moja ni ya siri, haina malipo, na inapatikana jimboni kote bila kujali hali yako ya uhamiaji. Sisi siyo polisi na hatutoi taarifa kwa polisi bila idhini yako.

Imetolewa na Washington State Office of the Attorney General.



Ripoti Chuki.
Pata Usaidizi.

Uhalifu wa Chuki ni Nini?

Hapa Washington, uhalifu wa chuki unaweza kuwa mambo kadhaa. Unaweza kuwa **shambulio ovu na la makusudi, uharibifu wa mali au tishio la kushambulia au kuharibu mali** dhidi ya mtu mwingine.

Uhalifu wa chuki hutendwa kwa sababu ya sifa ambayo mtu huyo anaonekana kuwa nayo au anayo kweli:

- Asili
- Rangi
- Dini
- Ukoo
- Asili ya taifa
- Jinsia
- Mwelekeo wake wa kijinsia
- Anavyojibainisha au utambulisho wake wa kijinsia
- Ulemavu wa kiakili, kimwiili au ufahamu

Uhalifu wa chuki ni jinai hapa Washington (RCW 9A.36.080).

Tukio la Upendeleo ni Nini?

Tukio la upendeleo ni hali ya **kuonyesha uhasama** dhidi ya mtu mwingine kulingana na sifa ambayo mtu huyo anaonekana kuwa nayo au anayo kweli:

- Asili
- Rangi
- Imani au dini
- Ukoo
- Asili ya taifa
- Uraia au hali ya uhamiaji
- Jinsia
- Askari aliyestaafu kwa heshima au cheo cha kijeshi
- Mwelekeo wake wa kijinsia
- Anavyojibainisha au utambulisho wake wa kijinsia
- Ulemavu wa ufahamu, kiakili au kimwili
- Matumizi ya mbwa mwenye mafunzo ya kuongoza watu au mnyama anayetoa huduma

Tukio la upendeleo halifikii kiwango cha kuwa uhalifu.

Mifano inajumuisha:

- Kutumia lugha ya matusi kulingana na sifa ambazo mtu anaonekana kuwa nazo.
- Kutengeneza picha au michoro ya kibaguzi au ya kudhalilisha.
- Kumdhihaki mtu kwa sababu ya ulemavu wake, mila na desturi zake, au matendo yake.